

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA
NACHINGWEA



Kumb. Na. LG.L.10/11/VOL.V/112

Tarehe 19 Aprili, 2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Kwa kuzingatia kibali cha ajira Kumb.Na. FA.97/228/01(TEMP)/06 cha tarehe 05 Aprili, 2023 kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea anawatangazia Watanzania wenye sifa na uwezo kuomba ili kujaza nafasi 04 za kazi.

1. MTENDAJI WA KIJIKI III NAFASI NNE (04)

SIFA ZA MWOMBAJI

- Muombaji awe amefaulu kidato cha nne (IV) au sita (VI) aliyefuzu mafunzo ya Astashahada/Cheti, "NTA level 5" katika fani zifuatazo:- Utumishi, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii, kutoka chuc chochote kinachotambulika na serikali.

KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI

- Afisa Masuluhwi na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- Kusimamia ulinzi na usalama wa raia na mali zao
- Kuwa Mlinzi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- Kuratibu Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake.
- Kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wataalam katika Kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.
- Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za vijiji.

MSHAHARA

Cheo cha Mtendaji wa Kijiji Daraja la III kina mshahara wa TGS B

Bomani, Mtaa wa Boma, S.L.P 291 Nachingwea, Simu: +255732 933 112, Nukushi: +255732 933 112, Barua pepe: ded@nachingweadc.go.tz, Tovuti www.nachingweadc.go.tz

MASHARTI YA JUMLA

- Muombaji awe Mtanzania mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono na kutumwa kupitia anuani iliyotajwa hapo chini.
- Muombaji ambatanishe nakala ya cheti cha kuzaliwa.
- Muombaji ambaye ni Mtumishi wa Umma na ana sifa za kuingilia katika kada tofauti na aliyonayo apitishie barua yake ya maombi kwa mwajiri wake kuthibitisha kuridhia.
- Muombaji aambatishe maelezo binafsi yaliyojitokeza (a detailed C.V) yenye anuani, namba za simu, pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za simu.
- Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma na mafunzo kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali:-
 - Cheti cha mthani wa kidato cha IV au VI.
 - Cheti cha mafunzo (professional).
 - Cheti cha kuzaliwa.
 - Picha moja (1) "passport size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- "Testimonials", "Provisional results", Statement of results", za kidato cha IV na VI HAVITAKUBALIWA.
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi zitapelekea wahuksika kushughulikiwa kisheria.
- Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe 04 Mei, 2023 saa 9.30 Alasiri.
- Watakaoitwa kwenye usaili majina yao yatawekwa kwenye tovuti ya Halmashauri (www.nachingweadc.go.tz)
- Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na yatumwe kwa njia ya posta kwa anuani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA
S.L.P 291,
NACHINGWEA.

Limetolewa na:-

Eng. Chionda A. Kawawa
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NACHINGWEA

NAKALA:- - Mbao za matangazo

- Tovuti: www.nachingweadc.go.tz